JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAMISEMI

Namba za simu ya Mkuu wa shule:-
0714 790 238
0628629621

S. L. P. 402,
DODOMA.

Msajili wa wanafunzi…0713950675

CSS/J. 1/VOL.VI/……..

Tarehe:-…….

Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi……..
S.L.P……

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI CHAMWINO HALMASHAURI YA CHAMWINO MKOA WA DODOMA MWAKA 2022.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022 tahasusi ya ……. Shule ya sekondari CHAMWINO ipo umbali wa kilometa 30 mashariki mwa mji wa DODOMA.

Usafiri wa basi kutoka mjini DODOMA unapatikana katika kituo cha mabasi SABASABA na nauri ni shilingi 1,400/=. Muhula wa masomo unaanza tarehe …,….,.2022. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …,…,2022. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ..., ..., 2022.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 **Sare ya shule kwa wavulana.**

(a) . Suruali ni rangi ya damu ya mzee yenye marinda. Isiwe ya kubana.
(b) . Shati ni rangi nyeupe ─ mikono mirefu.
(c) . Viatu vyeusi vya ngozi ─ vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi.
(d) . Socks jozi tatu ─ rangi nyeusi.
(e) . Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.
(f) . Sweta (linapatikana duka la shule kwa Tsh. 12,000/=)

2.2 **Sare ya shule kwa wasichana**.

(a) . Sketi ni rangi ya damu ya mzee. Iwe na mshono wa linda box (mshono kama sketi za masista wa kikatoliki), ndefu kuvuka kifundo cha mguu (Enka).
(b) . Shati ni rangi nyeupe ─ mikono mirefu.
(c) . Viatu vyeusi vya ngozi ─ vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi.
(d) . Socks jozi tatu ─ rangi nyeupe.
(e) . Kijuba (Hijab) kwa wanafunzi wa kiislamu ─ rangi nyeupe.
(f) . Sweta (linapatikana duka la shule kwa Tsh. 12,000/=)

2.3 **Sare za michezo**

(a) . T-shirt ya rangi ya kijani kwa wavulana na wasichana. Zisiwe na picha wala maandishi yoyote.
(b) . Track rangi nyeusi kwa wavulana, na rangi ya bluu kwa wasichana.
(c) . Raba za michezo.

2.4. **Nguo za kushindia (Shamba dress)**

(a) . T-shirt rangi ya bluu kwa wavulana na rangi nyekundu kwa wasichana (Zinapatikana duka la shule kwa Tsh. 15,000)
(b) . Suruali nyeusi zenye marinda kwa wavulana.
(c) . Sketi nyeusi zenye marinda kwa wasichana.

3. Ada na michango ya shule.

3.1 **Ada ya shule**

Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi **70,000.00** kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000.00 kwa mwanafunzi wa bweni kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja.

- Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule Na **51701100051 NMB**.
- Jina la akaunti ni ***CHAMWINO SECONDARY SCHOOL RUZUKU AC.*** (***Tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye pay-in-slip. Pay-in-slip isiyo na jina la mwanafunzi haitapokelewa***).
- **N.B:** Malipo ya **ADA** yafanyike kupitia akaunti hii tu, na si vinginevyo.

3.2 Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

(a) . Shilingi 10,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
(b) . Shilingi 5,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
(c) . Shilingi 20,000/=kwa ajili ya taaluma.
(d) . Shilingi 30,000/=kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
(e) . Shilingi 15,000/= kwa ajili ya Bima ya afya.
(f) . Shilingi 15,000/= mitihani ya nje ya kujipima.
(g) . Shilingi 5,000/= fedha ya tahadhari (haitarejeshwa).

- Michango hii ilipwe kwenye akaunti ya shule Na. **52810006441 NMB.**
- Jina la akaunti ni ***SHULE YA SEKONDARI CHAMWINO EK.***

(***Tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye pay-in-slip. Pay-in-slip isiyo na jina la mwanafunzi haitapokelewa***).

3.3 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

(a) . Ream ya karatasi mbili (02) kwa mwaka.
(b) . Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
(c) . Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
(d) . Scientific calculator.
(e) . Godoro kwa wanafunzi wa bweni (**Aje nalo**).
(f) . Mashuka jozi 2 (Yanapatikana duka la shule kwa Tsh. 16,000/=), blanketi 1, foronya 1, chandarua 1.
(g) .Vyombo vya chakula (sahani, bakuri, kijiko, na kikombe).
(h) .Ndoo mbili (02) ndogo (lita 10) zenye mifuniko.
(i) . Fagio ya kukaushia Maji (Plastic Floor Squeezer), jembe, kwanja, mifagio ya ndani na nje.
(j) . Dawa ya kusafishia choo (aro) lita moja.

4. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(a) .Wizi.
(b) .Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
(c) .Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(d) .Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(e) .Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
(f) . Kusuka nywele kwa mtindo wowote. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
(g) .Kufuga ndevu.
(h) .Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(i) . Uvutaji wa sigara.
(j) . Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
(k) .Kupata ujauzito au kutoa mimba.
(l) . Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(m) . kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(n) .kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(o) .kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(p) .kudharau bendera ya taifa/kengele.
(q) .kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
(r) . Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

N.B. Mwanafunzi asije na simu shuleni kabisa. Ni marufuku.

5. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU.

(a) .Fomu ya uchunguzi wa Afya (medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya serikali.
(b) .Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) .Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
(d) .Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuelni pamoja na namba zao za simu.

6. Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHAMWINO

Saini ya mkuu wa shule…….

Jina la mkuu wa shule.... ***NAMGA C. NAMGA***
Namba za simu:- ***0714 790 238/0628 629 621***

Mhuri wa mkuu wa shule…….

SHULE YA SEKONDARI CHAMWINO
FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI
HABARI ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la baba……
2. Kazi yake……
3. Jina kamili la mama…….. ……..
4. Kazi yake……
5. Jina kamili la mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake)……..……
6. Kazi na Anwani ya Mlezi…….. ……..
7. Nyumbani kwa baba (alipozaliwa mtoto)…….……..

   Kijiji/Mtaa…….…… Wilaya……..……
   Kata…… Mkoa……
   Tarafa…….

8. Anwani ya mahali pa kazi ya baba……..…… ……
9. Nambari ya simu……..……..……..
10. Anwani ya mahali pa kazi ya mama……... ……...…
    ……..……..……...
    Nambari ya simu……..……..……
11. Anwani kamili ya nyumba ambapo mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo
    …….. ……...

12. Mimi……..(Baba/Mama/Mlezi wa mwanafunzi .....Nathibitisha kuwa taarifa zilizotolewa hapo juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo, na kuwa nitawajibika kumhudumia gharama zote zitakazohitajika akiwa shuleni.

NB: Nguo za nyumbani haziruhusiwi kuja nazo shuleni.

Tarehe……. Saini……

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants.

Full name…… age……

Sex……..…… year…….....

1. Blood count (red and White)…….....
2. Urine analysis Test……
3. Syphilis Test…….....
4. T. B. ……
5. Eye Test ……..
6. Ears ……..
7. Spleen ……
8. Abdomen ……

N.B. Pregnancy test for girls is necessary.

ADDITIONAL INFORMATION e.g. Physical impairment, family disease, chronic infection etc.

……

……

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above.

…….. ……..…….

Name and Designation Signature and Official stamp

…… ……

Station **Date**

NOTE:

1. Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.
2. The dully-filled form must be handed to the Head of the school during registration week; under no circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.